WA KIPEKEE

Na tuendelee kusimama kwa muda kidogo. Bwana wa thamani, tunakuja kwenye uwepo Wako wa Kiungu tena kwa njia ya maombi; kwanza, kutoa shukrani kwa yale yote ambayo umetutendea, na kwa ajili ya upendo mkuu mioyoni mwetu kwa ajili Yako na kwa Neno Lako. Bwana, watu hawa, usiku huu, ambao nawapenda kwa moyo wangu wote, wamejitolea na wakaja kuketi katika chumba chenye joto, na kadhalika, kwa maana wao wanalipenda Neno Lako.

2 Nasi tumekuja kuwaombea wagonjwa, usiku huu, Bwana, na walio wahitaji. Na kusiwe na mtu aliye mnyonge miongoni mwetu mwishoni mwa ibada hii. Wajaze kwa ajili ya uaminifu wao, Bwana. Nena nasi kupitia Neno Lako, na utupe nguvu, Bwana, tunapoenda, huku tukichukua shutumu. Ni majaliwa ya jinsi gani kufanya jambo hili! Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina. Mwaweza kuketi.

3 Nisingepata maneno, bila shaka, kutoa shukrani zangu kwa kundi kama hili la watu, ambao wangekuja na kuketi katika jengo hili. Nataka kusema, ya kwamba, kesho . . . Ama, tutaenda kule Topeka, Kansas, kwa ajili ya mkutano unaofuata, na huo utamalizika Jumapili inayofuata. Kisha tutaenda, kutoka hapo, huko Philadelphia.

Na, sasa, tunakusudiwa kwenda ng'ambo, huko Kenya, na Tanganyika, na Uganda, kwenye ma—makabila kule ndani. Nao wana maasi madogo sasa ya Mau Mau. Siwezi kuingia kule kama mmishenari, bali nitajaribu kuingia kama mwindaji. Niingie, nao wanaitayarisha.

4 Kwa kawaida, mimi huingia mle kama mmishenari kisha nikaenda kuwinda, wakati huu ninaenda kana kwamba ninaenda kuwinda, kisha niwe mmishenari. Kwa hiyo, kule—kule, njia yo yote ya kuingia kule kuwafikia. Na Ndugu Mattsson-Boze yuko kazini, akijaribu kuniingiza, kutayarisha safari ambapo nitaingia niende kuwinda. Vema, kisha, naja katika safari hii, halafu yeye atasema, "Ndugu yetu Branham yuko nchini." Ashuke aende kwenye ubalozi, "Ni sawa kama tukifanya mkutano mdogo tu hapa?" Mnaona? Jambo hilo linaianzisha basi, nasi tuifanye iendelee mbele. Kwa hiyo hatujui kama itakuwa hivyo, kama tutaweza kufanya jambo hilo, ama hatutaweza. Tunajaribu. Nami nimemwomba Bwana, kama jambo fulani likitukia kwamba hawezi, basi itakuwa ni ishara kwangu kwamba ninapaswa kuja hapa Jeffersonville na kuhubiri zile *Baragumu Saba*, mnamo mwezi wa Julai ama Agosti, mahali fulani pale.

5 Halafu, kama tukifanya hivyo, tunaona leo, tutajaribu kukipata chumba hiki cha shule hii hapa ambacho kimebaridishwa, kwa kuwa kitakuwa kizuri sana na baridi kidogo. Kinakaa watu elfu moja mia tano hadi elfu moja mia nane. Nacho kimebaridishwa, mahali papya kabisa, yapata tu miraba mitano juu ya mahali hapa. Na wakati mmoja tulipaomba, nao hawangeturuhusu kupapata. Ndipo yule mtu ambaye hangeturuhusu kupapata alifukuzwa kwenye halmashauri. Kwa hiyo sasa, mtu aliyeko sasa anasema tunaweza kupapata wakati wo wote tutakao. Kwa hiyo tuna—tunafurahi sana kupapata. Na kwa hiyo huenda tukaweza kupapata sasa, na wakati fulani Julai, nasi tuna ninino . . . Ni wangapi wangekuwa wakiomba, kama Bwana akipenda sasa, kama kitu fulani kikitukatalia? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

6 Mnajua, mimi napenda Arizona. Ni nchi ya ajabu. Daima nimetamani kuwa kule.

Tafadhali vuta hiyo kidogo, Ndugu Ben, kama ukiweza, kama ni- . . . Loo, hiyo . . . Naam, bwana. Naam. Ama, sijui ni nani, ataifungulia kidogo tu, maana ninasikika kutoka hiyo ninino sana . . . [Mtu fulani anasema, "Kanda, ndugu."—Mh.] Unasemaje? ["Hizo ni kanda tu."] Loo, kanda tu. Loo, hii hapa ile nyingine hapa. Nasikitika. Haya basi, Ndugu Ben. Kwa hiyo mimi . . .

7 Nikirudi kutoka Arizona, nikija hapa, inanifanya nipwewe sauti kidogo, kwa sababu ya badiliko ya hali ya hewa. Hapa tuna yapata themanini na saba hadi tisini, na wakati mwingine asilimia mia moja, unyevu. Na kule hufikia sifuri, halafu wakati mwingine, kwa wastani, moja katika ishirini ya asilimia moja ya unyevu. Unaishi tu chini ya hema ya oksijeni. Kisha unatoka chini ya hiyo, ukaja hapa, unajua jinsi inavyoleta tofauti kubwa kwako. Kwa hiyo inakusumbua katika sauti, na kadhalika.

Ivute mahali ilipokuwa, tafadhali, Ndugu Ben. Nilifanya kosa nilipoivuta nikaitoa. Nilifikiri ilikuwa hivyo, bali *hapa* ndipo walipoiweka.

8 Sasa tuombeeni, kila mmoja wenu. Ninawathamini. Billy alikuwa akiniambia juu ya mtu fulani aliyetuletea kikapu kimoja cha maembe, na zawadi dogo tu ambazo ninyi . . . Siwezi kuwashukuruni vya kutosha. Si—sijui jinsi ya kufanya jambo hilo. Nami na—najisikia sistahili sana kuchukua vitu kama hivyo kutoka kwenu. Naomba ya kwamba Mungu atawabariki, nami najua atafanya hivyo, kwa maana alisema, "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu Zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi." Naye Mungu atawabariki, nina hakika.

9 Na Arizona ikiwa nchi nzuri namna hiyo, kuna kitu kimoja ninachokikosa, hicho ni, ninyi nyote. Hiyo ni kweli. Ninawakosa ninyi nyote. Si—sijali ninapokwenda, ni—ni . . . si, si ninyi. Nina marafiki, kila mahali ulimwenguni, bali si—si ninyi nyote. Kuna

kitu fulani kuhusu kundi hili dogo ambalo lina ninino tu… Sijui. Mimi huwafikiria.

10 Na kule Tucson, ni mji wa kitalii, mwajua, na makanisa yanazozana, mwajua. Kwa namna fulani ni vigumu. Si kwa kiroho sana; na, kwa maana kuna mashindano, ni makali sana; na inafanya jambo hilo kuwa gumu. Kama ningewapata ninyi nyote, na kanisa, kisha tuishi kule, nadhani ingekuwa sawa. Mnaona? Lakini nafikiri, mradi hili linadumu kuwa kanisa, nanyi nyote mngali mnakuja, ningali nitakuwa hapa, hata Yesu atakapokuja.

11 Kwa hiyo niombeeni, kama nilivyosema muda kidogo uliopita, sitaki kulirudia, bali ninapofika mbele yenu, ni—ninakuwa na wasiwasi, na ninapata huzuni, kisha nashikwa na upendo wa haraka, na mwepesi wa hasira, pia. Ndivyo nilivyo, kwanza, kwa hiyo mimi…inanifanya kuhangaika sana ndani yangu. Bali kujua ya kwamba mahali po pote niwezapo kwenda…sina ku—kundi fulani ulimwenguni, nilijualo, linaloshikamana nami kama kundi hili. Mungu na—na ajalie tuwe wasioweza kutengana sana, hata, katika Ufalme ujao, naomba kwamba tuwe huko pamoja; ombi langu.

12 Nikiketi hapa mlangoni, nikizungumza na Bill Dauch muda kidogo tu uliopita kabla ya kumwongoza mtu fulani kumrudia Kristo, tena, katika chumba kile kingine. Bali nikiketi pale na kuzungumza naye, umri wa miaka tisini na moja, yeye alisema, "Na—najisikia mnyonge. Macho yangu si kama yanavyopaswa kuwa."

Nami nafikiri, miaka michache iliyopita, nilimjia wakati alipokuwa ameugua ugonjwa mbaya wa moyo na kuziba moyo, alikuwa yuafa. Na daktari yule yule aliyekuwa anamtibu, aliyesema kwamba asingepona, daktari huyo amekufa. Na huyu hapa Bill Dauch ameketi, manaona, mwenye umri wa miaka tisini na moja. Nikasema, "Bill, huna faida duniani kadiri ya kufanya kazi na mambo kama hayo. Bali naomba jambo hili, 'Mungu na akupe nguvu,' kwa sababu unaipenda mikutano hii sana." Huyo mtu mwenye umri wa miaka tisini na moja huvuka nchi hii kwa motokaa, joto, kukavu, baridi, ubaridi, cho chote kile, kusikia Neno. Mungu na ambariki shujaa huyo. Sasa mimi sijaninino…

13 Nina udhuru mmoja zaidi, wa kuwaweka jinsi nilivyofanya asubuhi ya leo, kwa masaa matatu. Nami sikuufanyia haki huo ujumbe, kwa maana niliufupisha, na kuacha sehemu yake, na kuruka sehemu yake, na kadhalika. Hiyo ndiyo sababu niliwaomba wasiisambaze hiyo kanda. Naomba niupate tena mahali ambapo pana baridi ama po pote pale. Na ni—ni—ningesikia Roho, bali ninawaangalia na kujua mnajipepea na kujua mnasikia joto, na—na jambo hilo hunirarua vipande-

vipande. Sitaki ninyi mteseke; na—nawatakeni mstarehe. Mnaona? Na jambo hilo hunisumbua.

14 Kama vile, nawaona wagonjwa; kama siwezi—kama siwezi kuwahurumia hao wagonjwa, siwezi kuwasaidia. Si—sina budi kuwahurumia. Na ni vivyo hivyo kwe—kwenu ninyi; si—sina budi kuwahurumia, la sivyo siwezi kuwa ndugu yenu. Mnaona? Si—sina budi kuwahurumia. Na, mimi hufanya hivyo; Mungu anajua kwamba hiyo ni kweli.

15 Na sasa, usiku huu, nitautoa kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa.

Nami nataka . . . watu, kuwabariki watu hawa, na Ndugu Collins, na Hickerson, Ndugu Neville, Ndugu Capps, wadhamini, na hao wote, kwa ajili ya ripoti nzuri ambayo imekuwa ikija, ya jinsi mlivyo na utaratibu, mkiliweka kanisa, na jinsi kila kitu kinaingia katika mahali pake panapofaa. Ninawashukuru ninyi watu. Mungu awabariki kwa kujaribu kutekeleza agizo. Na barua baada ya barua huja huko Tucson, kwangu, "Ndugu Branham, si kama ilivyokuwa. Ni tofauti sana, kuhisi kwenye baraka sana kwa Uwepo wa Mungu." Nami—nami ninashukuru kwa ajili ya jambo hilo. Bwana awabariki daima!

16 Halafu, sasa, usiku huu, nilikuwa nikisoma hapa katika Maandiko mahali padogo, i—ili kwamba labda nitoe maneno machache, kunena na kusoma Andiko, halafu labda Maandiko kadha, kisha nizungumze nanyi muda kidogo ndipo niwaombee wagonjwa. Si zaidi ya muda kidogo tu; ninatazama ile saa, nami nitajaribu kumaliza mapema iwezekanavyo. Bali nafikiri wakati kundi la watu limekusanyika pamoja, bila kusoma Neno ama kufanya jambo fulani, mawaidha fulani, mkutano huo hautakuwa umekamilika.

17 Wengi wenu mlingojea. Wengi wenu mna maili kadha za kusafiri usiku huu. Jinsi ninavyopenda jambo hilo! Jinsi ninavyotazama na kumwona kila mmoja, nami ninafikiria kuhusu . . . Kule Arizona, nafikiri, "Nitakapomwona tena, nitashuka niende nikampe mkono na kuikumbatia shingo yake." Nanyi hapa mmeketi hapa, na ni nani, ni wapi ninapoweza, mwajua? Sijui nianze na nani . . . na ni yupi, na jinsi ya kutoka huko. Bali, naam, nawapenda. Mungu anawapenda, pia.

18 Sasa nafikiri, kama sijakosea, kama sina A—Andiko lisilo sahihi hapa, nataka kusoma kutoka Wakorintho wa Kwanza, sura ya 1, kuanzia na aya ya 18, na pia tusome Wakorintho wa Pili 12:11, kuchukua fungu la maneno. Sasa kama naweza kuyapata hayo upesi sana, kisha tutasoma, kisha tuombe na kuanza mara moja, kuwazungumzia tu kwa dakika chache juu ya somo dogo. Katika Wakorintho wa Kwanza, sura ya 1, kuanzia kwenye aya ya 18.

> *Kwa sababu* kuhubiriwa kwa *neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuzi, bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu za Mungu.*
>
> *Kwa kuwa imeandikwa, Nitaiharibu hekima yao wenye hekima, na akili zao wenye akili nitazikataa.*
>
> *Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mleta hoja wa zamani hizi? Je! Mungu hakuifanya hekima ya* ulimwengu *kuwa ni* upumbavu?

Naweza kunukuu hayo tena? "Mungu hakuifanya hekima ya ulimwengu huu kuwa ni upumbavu?" Hekima ya ulimwengu huu ni nini basi? Upumbavu.

> *. . . Je! Mungu hakuifanya hekima ya dunia hii kuwa ni* upumbavu?
>
> *Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa* waliokwisha kuamini *kwa upuzi wa lile Neno linalohubiriwa.*

Naweza kusoma aya hiyo tena? Sikizeni kwa makini.

> *Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neno lililohubiriwa.*
>
> *Kwa sababu Wayahudi wanataka ishara, . . . Wayunani wanatafuta hekima;*
>
> *Bali sisi tunamhubiri Kristo, aliyesulibiwa; kwa Wayahudi ni kikwazo, kwa Wayunani . . . upuzi;*
>
> *Bali kwao waitwao,* Myahudi *kwa* Myunani*, ni Kristo, nguvu za Mungu, na hekima ya Mungu.*
>
> *Kwa sababu upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya* mwanadamu*, na udhaifu wa Mungu una nguvu zaidi ya* mwanadamu.

19 Na katika Wakorintho wa Pili sura ya 12, aya ya 11, Paulo akizungumza,

> *Nimekuwa mpumbavu* katika kujisifu*, ninyi mmenilazimisha. Maana ilinipasa nisifiwe na ninyi; kwa sababu sikuwa duni ya* mtume *walio wakuu kwa lo lote, nijapokuwa si kitu.*

20 Na tuombe. Bwana Yesu, ongeza kwa maneno haya machache, usiku huu, ambayo yamenenwa katika siku zilizopita, na mtume mkuu Paulo, ili kwamba tupate kufanikiwa kwa kuyasikia usiku huu, katika kuyatumia katika maisha yetu, kusudi tupate kuwa ka—kazi ya mikono ya Mungu, waliofanywa kwa njia ambayo Yeye angetaka sisi tuwe. Kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

21 Nitahubiri usiku wa leo kwa dakika chache, Bwana akipenda, juu ya somo la: *Wa Kipekee*. Naam, hilo ni somo la kijinga na la kifidhuli kuchukua, bali hilo, nafikiri, kwa kadiri fulani lingeliweka jinsi ninavyotaka kulisema.

22 Mwajua, kuna mambo mengi sana, leo, ambayo watu huwa *wa kipekee* kwayo, tunavyosema. Na tamshi hilo, kama mtu ye yote hajawahi kulisikia, linamaanisha mtu "asiye na kifani," mtu ambaye ni "wa kipekee" kwa jamaa mwingine. Na hapana shaka kwamba wengi wetu ni wa kipekee, mmoja kwa mwingine.

23 Naam, basi, nilikuwa nikishuka kwenda barabarani wakati mmoja huko Los Angeles, California, nami nikamwona mtu wa kipekee sana, akitenda mambo yasiyo ya kawaida. Naye alikuwa akitembea barabarani, si akirandaranda, lakini alikuwa tu kama kwamba anapunga hewa wakati wa alasiri. Nami nikaenda upande wa pili wa ile barabara, nione alichokuwa anafanya. Kila mtu alikuwa anageuka, akimcheka, kwa sababu ya upekee wake.

Niliona kwamba alikuwa na maandishi yaliyoning'inia upande wake wa mbele. Ndipo nikafikiri ningeona kile kila mtu alichokuwa anacheka, mtu huyu wa kipekee, mtu asiye na kifani. Na kwa hiyo yeye alikuwa . . . Niliona kwamba wakati watu walipomwangalia, walimcheka, na—na, bali alionekana kana kwamba alikuwa na aina tofauti ya tabasamu, tabasamu la kuridhika. Hizo tabasamu zingine watu walikuwa wanampa zilikuwa kama za kumdhihaki, bali alionekana kana kwamba ameridhika katika yale aliyokuwa anafanya.

24 Vema, hayo ni mambo mengi ya kuwazia, wakati mtu ameridhika, na yale anayofanya ni sahihi. Ingawa yeye ni wa kipekee kwa mtu mwingine, iwapo ameridhika kwamba anayofanya ni sahihi, basi acha adumu nayo.

Na nilipomkaribia maskini mtu yule, nikaona juu . . . kifuani mwake hapa, kwenye kijikaratasi chenye maandishi ama ubao, iliandikwa, "Mimi ni mpumbavu," na hapo chini, palikuwa na, "wa Kristo." "Mimi ni mpumbavu," katika herufi kubwa; huku chini, kasema, "wa Kristo." Na kila mtu alikuwa anacheka jambo hili.

25 Na maskini mtu huyu aliposhuka akijisukumiza kupitia katika umati wa wenye kudhihaki na kumpigia makelele, niligeuka kuangalia kilichokuwa kwenye mgongo wake. Basi kulikuweko na alama ya kuuliza kubwa mno mgongoni mwake, na huku chini, ilisema, "Basi wewe nawe u mpumbavu wa nani?"

26 Vema, ni—nilifikiri alikuwa na jambo fulani hapo, mnaona, bali alionekana ameridhika kwamba yeye angeweza kuwa mpumbavu wa Kristo. Na hivyo ndivyo Paulo alivyosema alikwisha kuwa, "mpumbavu" kwa ajili ya Kristo.

27 Ndugu Troy, wa Wafanyi Biashara wa Injili Yote, rafiki msiri wangu, ye—yeye ni mkata nyama. Basi aliambukizwa na viini mkononi mwake, kutokana na kukata nyama ya nguruwe wakati mmoja. Baadhi ya watu wanaojua, ama wanawake, wanaweza kujua viini hivyo vilikuwa nini; bali vita—vitakula. Kwa hiyo, kusudi wapate kuyaokoa maisha yake, walilazimika ku—kumkata vidole vitatu. Naye ana vidole viwili tu katika mkono mmoja, bali hata hivyo yeye angali ni mchinja nyama.

28 Na kulikuwa na maskini Mjerumani aliyefanya kazi pamoja naye katika—katika duka la nyama, kule Los Angeles, kwa hiyo aka—akashikilia kujaribu kumwongoza maskini Mdachi huyo kwa Kristo. Naye alisema ya kwamba alikuwa "Muluzeri," naye hakuwa na neno. Yeye aliridhika ya kwamba alikuwa Mkristo, kwa sababu alikuwa mfuasi wa kanisa la "Kiluzeri," kama alivyolitamka. Kwa hiyo usiku mmoja Ndugu Troy alikuwa na majaliwa ya kumpeleka kanisani.

29 Jina lake aliitwa Henry. Na Henry, katika Kijerumani, ni "Heinrich," na kwa hiyo wao walimwita "Heini." Mmesikia tamshi hilo. Yeye akasema, "Heini, vipi kuhusu kuenda nami kanisani usiku huu?"

30 "Vema," akasema, "naaamini nitaenda." Kwa hiyo akashuka akaenda kwenye mkutano wa mtindo wa kale mahali ambapo walikuwa na mkutano wa maombi, na kwa kweli akasadikishwa kabisa, kisha akampa Kristo moyo wake.

Loo, siku iliyofuata, maskini Mdachi huyu alikuwa anafurahi. Kila baada ya muda kidogo angetembea jengoni, mikono yake hewani, akisema, "Mungu asifiwe! Asante, Bwana Yesu!" naye akavutia usikivu wa watu wote, wote hao.

31 Unaona, yeye akawa wa kipekee kwa mlolongo wote wa wakata nyama. Naye angekuwa akikata nyama, halafu angeanza kufikiria juu ya Bwana, kisha angeanza kulia. Angekiweka kisu chini, na kutembea huku na huko kwenye yale marefu ya jengo, si kwa kutokuweza kujizuia, bali akiendeleza mapenzi tu na Kristo, akisema, "Loo, jinsi ninavyokupenda, 'Jesu!'" Unajua, huku anatembea huku na huko.

32 Naye bosi akaja pale na kumwona akifanya jambo hili, na alipokuwa anakwenda akitembea, huku analia. Basi, yule bosi, yeye hakumwona bosi; alikuwa anafikiria juu ya Yesu. Kisha akaanza kushuka, huku mikono yake imeinuliwa juu hewani, na machozi yanatiririka mashavuni mwake, akisema, "Ee Mungu, jinsi ninavyokupenda!"

Ndipo yule bosi akasema, "Heini, nini kimekupata lakini?" Akasema, "Kila mtu kwenye—kwenye mlolongo huu wote anazungumzia jambo hilo. Nini kimekupata, Heini lakini?"

33 Maskini yule Mdachi akasema, "Loo, bosi!" Akasema, "Mungu atukuzwe, niliokoka!"

Akasema, "Ati ulifanya nini?"

Akasema, "Niliokoka!" Akasema, "Nilishuka nikaandamana na Ndugu Troy kwenda hapa kwenye misheni ndogo, nami ni—nikaokoka. Ndipo Yesu akaingia moyoni mwangu, nami nimejaa upendo!"

Yeye akasema, "Hapana budi ulishuka ukaenda kwenye kundi lile la nati."

34 Yeye akasema, "Naam!" Akasema, "Mungu atukuzwe!" Kasema, "Mungu ashukuriwe kwa ajili ya nati!" Akasema, "Unajua, ukichukua motokaa inayoshuka ikija barabarani, nawe utoe nati zote ndani yake, huna kitu ila lundo la vitu 'shaghalabaghala!'"

35 Vema, sijui ila kwamba maskini yule Mdachi alikuwa karibu sahihi. Kutoa nati zote? Nati ndizo zinazoishikiza pamoja. Nami nafikiri hizo ndizo zinazolishikilia kanisa pamoja wakati mwingine, zinazoushikilia ustaarabu pamoja.

36 Sasa, nikishuka kuja kutoka matembezini huko Prescott, siku chache zilizopita, nilikuwa ninaangalia jangwa hilo na kuona jinsi ambavyo kutoka huko Phoenix wao wana Bustani za Kijapani, nao walikuwa na maua humo ndani, maua mazuri. Ambapo, nilipokuwa mvulana mdogo kule, nilichunga ng'ombe kule chini kote. Hao ng'ombe, hakukuweko na nyasi, kwa hiyo walikula maharagwe ya mipungate na kadhalika.

37 Kisha nikaona ya kwamba wa—wanakuza mimea kwa matumizi ya jangwa. Na katika jangwa tunapata hiyo, mipungate na maua. Na kwenye nyumba yangu kule, ama ile nyumba tunayopangisha; Dada Larson, nafikiri alikuwa hapa asubuhi ya leo, nilimwona. Naye ana tuta la maua nje ya—ya nyumba; udongo. Kila kitu kule ni changarawe, kwa hiyo alikuwa na udongo mchache kwenye tuta kubwa katika kila upande wa ile nyumba. Na kila asubuhi sina budi kuamka na kuyamwagia hayo maua maji. Nisipoyamwagia maji, yatakufa. Nayo yataninino . . . Halafu, tena, sina budi kupata madawa na kuyapiga, yasipatwe na chawa; wadudu watayala.

38 Kisha unaondoka unaenda kidogo mbele ya mahali hapo, futi thelathini kutoka hapo, kuna maua yanayokua, na huko jangwani yanakua. Nawe ungechimba futi ishirini na ingekuwa kama kipipa cha poda; hakuna kitu ila vumbi, na hakuna maji hata kidogo. Na ni nani anayeyapiga dawa? Mnaona?

Haya yaliyo katika shamba la maua, usipoyapiga dawa na kuyamwagilia maji, mchwa na wadudu, chawa, watayala. Bali chawa hawawezi kuyagusa yaliyo kule jangwani, na wala halihitaji kubembelezwa na kumwagiliwa maji kila siku; hilo limetokana na muumbaji. Haya hapa yametokana na kuchanganyisha mbegu.

39 Nami nafikiri ya kwamba, leo, sababu ya Ukristo kuwa, kwa watu, nati; ni kwa sababu tuna kundi la miigo na si Wakristo halisi, kundi ambalo halina budi kubembelezwa kitoto na kupigwa dawa, ili lipate kukaa kanisani.

40 Naweza kuwazia Kanisa la kwanza kabisa, walivyokuwa, na kulilinganisha na miigo hii leo. Hii ingekuwa miigo duni ya kile Kanisa la kwanza lilivyokuwa, hao waaminio washupavu wa Mungu, wenye Roho Mtakatifu. Hukuwabembeleza kitoto. Haikukubidi kuwapapasa na kuwaambia ya kwamba ungewaingiza ndani ya *hili*; na wakichoshwa na lile, huenda kwa lingine; nawe utawafanya mashemasi iwapo watakuja hapa na kuliacha hili lingine. Huo ni mwigo wa kuchanganyisha mbegu.

41 Nilikuwa nikifikiria juu ya ile picha ya asili iliyochorwa na Michelangelo, naamini, ya "Meza ya Bwana ya Mwisho." Nafikiri aliichora. Unatambua hiyo picha ya asili ingekugharimu nini? Ingekuwa maelfu yasiyohesabika ya dola, hayangeigusa hiyo ya asili, kwa maana hainunuliki. Ina gharama ya juu sana! Bali unaweza kununua nakala yake rahisi kwa kama dola mbili.

42 Hiyo ndiyo sababu leo watu hawawezi kuelewa ushupavu wa waamini halisi, na wa kweli. Wao wanakuwa nati. Mnajua, ulimwengu unakuwa katika utaratibu mno hata ikawa baada ya muda kidogo huna budi kuchukua nati kuutengeneza. Inachukua mtu fulani kujitokeza ambaye ni tofauti kidogo, naye ni nati kwa kizazi hicho. Nilikuwa nikiwaza hivi majuzi, ni nani awezaye?

Ni nani siku hizi ambaye si nati? Wewe ni nati ya mtu mwingine. Ninaamini ulimwengu unaingia kichaa kabisa. Ulijua ni wakati ambapo watu hawawezi kubainisha kati ya mema na mabaya, au ukweli au uongo?

43 Unajua wanasiasa hawawezi kubainisha kati ya mema na mabaya? Unawaona wakinyamaza juu ya kura hii ya kuirudisha Biblia kanisani ama. . . Kuirudisha Biblia shuleni? Wao hawajui siasa zitaelekea upande gani. Wazia hilo! Sijui jinsi ilivyo Indiana sasa, bali katika mkoa wa Arizona si halali kuisoma Biblia shuleni. Nafikiri ni jambo lile lile Indiana, karibu Marekani nzima, kwa sababu mwanamke fulani kafiri alibadilisha utaratibu wote. Pia, kumbuka, si halali kuisoma Biblia katika shule zetu za serikali, bali kodi za waamini zinasaidia ukafiri kufunzwa shuleni.

44 Siasa. Tunahitaji Abraham Lincoln mwingine. Tunahitaji Patrick Henry mwingine. Tunahitaji Mwamarekani ambaye anaweza kusimama madhubuti haidhuru siasa ziko wapi, na kuita kweli, "kweli," na kosa, "kosa."

45 Mnajua wahubiri siku hizi hawawezi kuamua ni lipi sahihi, Neno la Mungu ama madhehebu ya kanisa? Hawajui wachukue

njia gani. Hawawezi kuamua kati ya ukweli na uongo. "Najua Biblia inasema jambo hilo, bali kanisa letu linasema..." Mnaona, watu hawawezi kuamua kati ya ukweli na uongo. Na kila kitu kilicho dhidi ya Biblia ni kosa. Neno la Mungu ni sahihi, na kila neno la mwanadamu ni uongo, ambalo liko kinyume. Na ukijaribu kusimama sasa katika wa—wa—wakati kama huo, na kutetea kweli, unakuwa nati.

Hebu tuwaite watu wachache.

46 Naweza kumwazia nabii Nuhu, katika siku ile kuu aliyoishi; wakati huo mkuu wa kisayansi ambao walijenga piramidi na masifiniksi, ambapo wangeweza kuthibitisha ya kwamba hakuna maji mbinguni, kwa utafiti wa kisayansi. Huyu hapa mzee anatokea kule, akasema, "Kutanyesha mvua kutoka mbinguni." Nuhu alikuwa nati kwa kizazi hicho. Yeye akawa nati.

47 Natuwazie juu ya Musa. Musa, wakati aliposhuka akaenda kwa Farao, kama tulivyonena asubuhi ya leo, na Musa akishuka akienda kwa Farao, na kusema, "Bwana alinituma nishuke nije nikawatoe watumwa hawa," huku ameshika fimbo mkononi mwake, dhidi ya jeshi kuu liliokuwa limeushinda ulimwengu mzima. Farao, katika ustadi wake wote wa kisayansi, alifikiri Musa alikuwa nati. Naam, alikuwa nati, kwao.

48 Naweza kumwazia nabii Eliya, katika siku yake kuu, wakati ule wakati wa fahari sana wa mtindo; wakati Ahabu na Yezebeli walipoutawala ulimwengu, kama ilivyokuwa, katika siku hizo; na ile mitindo yote na kadhalika ambayo Yezebeli alitaka kuvaa, na jinsi alivyowafanya wanawake wote kuvaa kama yeye, na vipodozi vyake, na kuendelea, mitindo yake, jinsi alivyojipamba. Na wakati mzee mmoja hafifu, kama Eliya, alipojitokeza na kusimama dhidi ya taifa zima; kwa Ahabu, yeye alikuwa nati. Hiyo ni kweli.

49 Amosi, yule nabii, alipokuja Samaria siku zile Samaria ilipokuwa kama Hollywood leo, hao wanawake barabarani, walivyovalia, na hata uzinzi wa hadharani, jinsi wanavyofanya yasiofaa na kuishi huko nje, wakiwaruhusu wanaume...

50 Karibu ni uzinzi wa hadharani, leo, moja kwa moja mbele yako. Nilienda mahali fulani hivi majuzi usiku, kutafuta kitu cha kula, na wavulana wadogo pamoja na wasichana kule juu wakikumbatiana na kubusiana sijui kama nini.

Na je! wajua, maskini dada yangu, ya kwamba huo kwa uwezekano ni uzinzi? Wakati mwanamume anapokubusu, yeye kwa uwezekano amefanya uzinzi na wewe. Hupaswi kumruhusu kamwe akubusu hata utakapoolewa, kwa maana zile tezi, tezi za kiume na za kike pia, zimo midomoni. Mnafahamu? Na wakati tezi za kiume na za kike zinapokutana, hata iwe ni wapi, kwa uwezekano umefanya uzinzi. Basi usimruhusu kijana akubusu hata lile shela litakapoondolewa usoni mwako nawe u mke wake.

Usifanye hivyo! Ni kufanya uzinzi. Ni kuchanganyisha tezi za kiume na za kike.

51 Kwa nini mwanamume hambusu mwanamume, mwanamke ambusu mwanamke, midomoni? Kwa maana tezi hazichanganyikani. Watoto huzaliwa kwa kuchanganyisha tezi.

Kwa hiyo karibu ni uzinzi wa hadharani tena, kila mahali. Angalia kwenye sinema na kila mahali unapoangalia, ku—kunyonyana ndimi na ku—kufanya yasiyofaa. Si ajabu uzinzi una—unaongezeka! Wanawezaje kufanya hivyo, huku wanajichafua kwa shahawa kwa kuwabusu hao wanawake mdomoni, wakijua ya kwamba huo ni uzinzi! Mungu hatakusamehe jambo hilo isipokuwa utubu.

52 Na sasa, wakati alipokuwa anakuja, huyu nabii mkuu, Amosi. Yeye anajulikana kama mmoja wa manabii wadogo kwa sababu hakuna mambo mengi sana yaliyoandikwa juu yake, bali alikuwa na Neno la Bwana. Naye akaangalia kwenye huo mji, wote umejiingiza . . . Kwenye bustani, wanaume wameketi huku wamewakumbatia wanawake, na wanawake wamewakumbatia wanaume, ni Hollywood ya kisasa tu! Naye akatembea kupitia mjini humo, akasema, “Mtatubu la sivyo mtaangamizwa!” Yeye alikuwa nati. Yeye alikuwa karibu amejitangaza mwenda wazimu, kwao.

53 Yohana Mbatizaji, alipojitokeza. Kwa madhehebu ya kidini ya siku hizo, yeye alikuwa nati. Yeye alikuwa na nafasi ya kuwa kuhani, kufuata nyayo za baba yake. Bali akakataa kufanya hivyo, kwa sababu Mungu alikuwa amemweka mbali na hizo kanuni za imani na madhehebu, kwa maana kazi yake ilikuwa muhimu sana. Yeye alikuwa amtangaze Masihi atakayekuja. Na wakati hakuwa na uhusiano wo wote na Mafarisayo, Masadukayo, ama wo wote wale, yeye alilikataa kundi lao lote, kisha akasema, “Msianze kusema, ‘Tunaye baba yetu Ibrahimu,’ kwa maana nasema ya kwamba Mungu aweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.” Kwa—kwa ulimwengu wa kidini wa siku zake, yeye alikuwa nati. Sawa.

54 Wakati Yesu alipojitokeza. Kwa watu wa kidini wa siku Zake, Yeye pia alikuwa nati. Kwa sababu, wao walisema, “Wewe ni Msamaria. Umerukwa na akili. Wewe ni mwenda wazimu,” kwa maneno mengine, “mtu mwenye kichaa.” Alikuwa hivyo, kwa watu, Bwana na Mwokozi wako.

Si ajabu, Paulo, aliyefunzwa na Gamalieli kuwa kuhani, nafasi siku moja kuwa kuhani mkuu. Na alipokuwa njiani akienda zake Dameski, alipigwa na kuangushwa na Nuru ya kimbinguni. Naye akainua macho yake, akiwa Myahudi, na alijua Nguzo hiyo ya Moto ndiyo iliyowaongoza watu wake. Yeye alisema, “Bwana, U nani Wewe?”

Naye akasema, “Mimi ni Yesu.”

55 Na wakati yeye alipoiacha elimu yake, akaiacha theolojia yake yote ambayo aliyokuwa amefunzwa shuleni, naye akawa mhubiri wa kawaida wa barabarani, yeye alikuwa nati. Alisema, "Nimekuwa mjinga."

56 Ndipo hao watu wakafikiri ya kwamba alikuwa mwenda wazimu, amerukwa na akili. Alimwambia Festo, "Mimi si mwenda wazimu." Yeye alimjua tu Bwana. Lakini kumjua Bwana katika kundi la wenye dini . . .

Natumaini hamtalikosa. Kumjua Yesu, siku hii, miongoni mwa kundi la kidini, wewe ni nati. Haijabadilika. Ningeweza kukaa sana juu ya jambo hili, bali na—nataka kuharakisha kwa ajili ya mstari wa maombi.

57 Martin Luther, maskini yule kasisi Mjerumani, aliyekuwa amechukua mkate wa ushirika siku moja, aliutupa chini kwenye vipandio, na kasema, "Huu si mwili wa Yesu Kristo. Huu ni mkate tu uliotengenezwa kule nyuma." Naye akatangaza, kwamba, "Mwenye haki ataishi kwa imani." Yeye alikuwa nati, kwa kanisa Katoliki. Wao wangaliweza kumuua kwa ajili ya jambo hilo, lakini, yeye alikuwa nati, nao wakamwacha tu. Bali, akawa nati, kwa kizazi hicho.

58 John Wesley, katika ile saa kuu ya ufisadi wa Uingereza. Ambapo, kama ufufuo wa Kiwesley haungalitokea . . . Ulimwengu mzima ulikuwa umepotoka, ufisadi kila mahali. Na kanisa la Kianglikana lilikuwa limeenda mbali sana hata hakukuweko na ufufuo tena; mawazo ya Ukalvinisti kama hayo! Ndipo John Wesley akajitokeza, na ne—neno la utakaso, kusafisha ufisadi. Akawa nati.

59 Nikimnukuu Bw. Wesley, wakati mmoja, katika kitabu chake. Alikuwa anashuka akija kwenye njia, ndipo mmoja wa watu wa kanisa la Uingereza . . . Wote walifikiri alikuwa na kichaa, kwa hiyo akasimama njiani. Bw. Wesley alikuwa mtu mdogo sana. Jitu hili kubwa mno lilifikiri linaweza tu kumpiga kofi limwangushe, kwa hiyo likasimama njiani. Bw. Wesley akapanda akaenda akasema, "Tafadhali, bwana, waweza kuondoka njiani? Nina haraka."

Naye yule Mwanglikana akasema, "Mimi simpishi mpumbavu."

60 Bw. Wesley kwa heshima akainamisha kofia yake, akamzunguka; kasema, "Mimi kila mara humpisha." Kwa hiyo, unaona, huyo ndiye aliyekuwa nati; mmoja alikuwa kwa ajili ya Kristo; yule mwingine kwa ajili ya kanisa.

Kwa hiyo, wewe u nati ya mtu mwingine, hata hivyo.

61 Wakati Wapentekoste walipojitokeza, miaka hamsini iliyopita. Walisema, "Hao watu wana kichaa!" Walikuwa nati, hiyo ni kweli, kwa kuwa walihukumu upotovu huo wote uliokuwa katika nyakati za kanisa wakati huo walipojitokeza.

Bali Wapentekoste wamefanya nini? Walirudi moja kwa moja kwenye matapiko walimotoka, moja kwa moja kwenye upotovu wa kimadhehebu. Mwajua nini? Wakati wa nati nyingine umewadia. Naam. Wakati wa nyingine umewadia. Hiyo ni kweli.

62 Angalia, nati, kabla hapajakuwepo na nati, kuna skrubu ya kuingia katika nati hiyo. Na hiyo nati haina budi kuingizwa kwenye skrubu hiyo; kama haiingizwi, haifai . . . Angalia. Wote walioingizwa, katika siku za—za Nuhu, walioingizwa kwenye ujumbe wa Injili; Nuhu, aliyekuwa nati, aliwavuta akawaingiza katika safina. Inategemea hesi zako ni nini, umeingizwa kwenye kitu gani. Kama umeingizwa ulimwenguni, watakuvuta. Kama umeingizwa kwenye Neno, litakuvuta. Inategemea umeingizwa kwenye kitu gani, ni nati gani utakayofuata.

63 Lakini Nuhu, akiwa nati kwa Neno la Mungu, nati kwa kizazi cha kisayansi na kwa wakati wa kidini alimoishi, yeye aliwavuta, ambao wangeokolewa, akawaingiza safinani. Amina. Hao waliokuwa wamekusudiwa tangu zamani, ile skrubu iliyotengenezwa kabla ya nati. Skrubu haina budi kuingizwa kwenye nati.

64 Kwa hiyo, Shetani, yeye ana baadhi ya skrubu na nati, pia, skrubu na nati za milki za ulimwengu huu.

Farao alikuwa nati tu kwa Nuhu, ama kwa Musa, kama vile Musa alivyokuwa kwa Farao. Farao, akiwa na maigizo yake yote ya uongo ya kisayansi, alikuwa amelivuta taifa lote akalileta kwake. Nuhu, kwa kuwa nati kwa Mungu, alilivuta kanisa akaliingiza kwenye nchi ya ahadi. Inategemea jinsi ulivyoingizwa. Yeye alilivuta kanisa akalitoa Misri; kama vile Nuhu alivyolivuta kanisa akalitoa ulimwenguni, hata kwenye safina. Musa alilivuta kanisa akalitoa Misri, akaliingiza kwenye nchi iliyoahidiwa na Mungu.

65 Yesu alisema. Sasa, iweni waangalifu, kwa maana hizi nati na skrubu zinafanana sana. Tazama tu hesi zake. Mathayo 24:24, Yeye alisema, "Karibu ingewapoteza walio Wateule."

Naam, Ma—Marekani na madhehebu yote ya ulimwengu yanahitaji nati.

66 Mmethodisti, Mbatisti, Mpresbiteri, wote wametawanyika katika *hili, lile*, na wote wanapigana. Na, hata hivyo, wote wameingizwa katika skrubu ile ile. Kwa hiyo Mungu amewapa skrubu, kisha akawatumia nati, Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Litawavuta wote pamoja. Hiyo ni kweli. Bila shaka litawavuta. Litawavuta pamoja, hilo Baraza la Ulimwengu.

67 Mnajua, imefikia, hapa si muda mrefu uliopita . . . Hakuna kinachoweza kutukia, tukio fulani, bila sababu. Wanawake wanataka kuvua nguo zao. Walitaka kuvaa kaptura. Walitaka kuendelea kuwa washiriki wa kanisa. Walitaka kuvaa hizi 'kini,' ama cho chote unachoviita vitu hivi. Wanataka kufanya jambo

hilo, na bado wangali wanataka kuwa washiriki wa kanisa; wanataka kupiga makelele, kupiga mayowe, na kucheza dansi; kuabudu, huko ni kuabudu.

68 Sasa, kama ningalikuwa na wakati, ningewathibitishia jambo hilo. Hiyo ni ibada ya ibilisi, kucheza dansi namna hiyo na kufanya mambo hayo. Naweza kuwathibitishia hilo, katika nchi za makafiri. Wao walitaka kuabudu, na kushikilia ushuhuda wao na bado wabaki kanisani. Kwa hiyo Mungu akawapa nati, mbili ama tatu za hizo; moja iliitwa Elvis Presley; moja, Pat Boone, na Ernie Ford; wanaweza kuimba nyimbo za kidini na cho chote kile, na bado adai eti yeye ni Mkristo. Ni nati. Haijatiwa kwenye Neno. Sawa.

Naam, nilisema nitamaliza katika muda wa nusu saa, na imekwisha.

69 Bali, sikiza, ulimwengu unahitaji nati. Ibilisi anahakikisha ya kwamba wanaipata. Wao tayari wametiwa kwenye hesi zake.

Lakini, wakati ulimwengu unapotiwa hesi kwa ajili ya nati, kuna watu wanaoitwa Bibi-arusi. Ametiwa hesi, pia. Kwa uhakika kama ninavyosimama hapa, Mungu atawatumia nati ambayo itamvuta Bibi-arusi atoke katika mchafuko huu, imwingize katika Uwepo wa Mungu. Itakuwa nati iliyotiwa hesi kwa Neno.

70 Mtoa lawama, siku chache zilizopita, aliniambia, kule chini Tucson. Alisema, "Unajua, watu wengine hukufanya wewe nati, na wengine wanakufanya mungu."

Nikasema, "Vema, jambo hilo liko sawa kwa namna fulani." Nilijua anajaribu kunilaumu. Mnaona?

71 Yeye akasema, "Watu wanafikiri wewe ni mungu."

72 Nikasema, "Vema, ninino tu . . . " Nilijua watu hawakufanya hivyo. Bali ni—nilijua yeye hakufahamu hilo, kwa maana alikuwa upande wa pili wa ngozi, mnaona. Kwa hiyo nilijua yeye hakufahamu, hakufahamu hilo. Kwa hiyo nikasema, "Jambo hilo haliko mbali sana na Neno la Mungu. Sivyo?"

Mnaona, kumfanya tu ajue—kumfanya tu ajue sisi hatukuwa tumepotea. Tulijua tulipokuwa tunasimama. Tunajua tulikuwa tumetweka matanga ya namna gani, na ni upepo wa namna gani ulikuwa unayavumia. Tunajua hesi zetu zilivyokuwa, na nati yetu ilivyokuwa. Nasi tunajua jinsi tunavyosimama.

Nikasema, "Hilo si kinyume cha Neno la Mungu, sana. Sivyo?" Nikasema, "Kumbuka, wakati Mungu alipokuwa anamtuma Musa ashuke aende kwa wana wa Israeli, Mungu alimfanya Musa mungu, hiyo ni kweli; naye akamfanya, pia, ndugu yake Haruni, nabii. Hiyo ni kweli. 'Manabii wote,' Yesu alisema, 'walikuwa miungu.' Wao hawakuwa miungu; wanadamu." Hiyo ni kweli. Mungu analimaanisha hivyo.

73 Sikizeni, Neno tunalohubiri na neno nililosema asubuhi ya leo, "Mungu akijificha nyuma ya ngozi, ngozi za pomboo, Mungu akijificha nyuma ya ngozi ya mwanadamu." Mnaona? Hivyo ndivyo alivyofanya. Mungu alipodhihirishwa ulimwenguni, Yeye alikuwa amejificha nyuma ya pazia, nyuma ya ngozi ya Mtu aliyeitwa Yesu. Yeye alikuwa ametiwa utaji na kujificha nyuma ya ngozi ya mtu aliyeitwa Musa, nao walikuwa miungu, si Mungu; bali walikuwa Mungu, yule Mungu mmoja, akibadilisha kinyago Chake tu, akifanya jambo lile lile kila wakati, akileta Neno hili. Mnaona, Mungu alilifanya jinsi hiyo. Yeye anajua ya kwamba binadamu hana budi kuona kitu fulani; kitu hicho kimo ndani ya kila mmoja wetu aliyezaliwa katika ulimwengu huu.

74 Kama nilivyokuwa nikiwaambia asubuhi ya leo, hakuna mtu aliyethubutu kumfuata Musa mle ndani. Mungu kamwe hajapata kushughulika na watu wawili. Yeye hujishughulisha na mmoja, kila wakati. Hakuna aliyepaswa kumwiga Musa. Ilikuwa ni mauti, mauti ya kimwili, kujaribu kumwiga, kuingia katika ile Nguzo ya Moto pamoja naye. Kwa hiyo watu wote hawajafanywa . . . Wewe hujazaliwa namna hiyo, kuvunja ukaingia katika hayo ya kimbinguni.

Lakini Mungu aliweka wengine duniani kumwakilisha Yeye, kama mabalozi kutoka Kwake. Na huyo balozi amechaguliwa, na Mungu, kuingia katika mambo makuu yasiyojulikana ya kimbinguni, na kutambua, na kuyaleta mambo ambayo akili ya kawaida haiwezi kuyaelewa. Inafanya wazi siri ya Mungu, inatabiri mambo yaliyopo, na mambo ambayo yamekuwepo, na mambo ambayo yatakuwepo. Ni nini? Mungu, Mungu nyuma ya ngozi, ngozi za binadamu. Kweli hasa.

75 Sam Connelly anaishi huko Tucson. Yeye alikuja hapa wakati mmoja, miaka mingi iliyopita, pamoja na Bw. Kidd, naye akaponywa; akiwa na vidonda vya tumbo kwa miaka mingi. Nilipotoka nikaenda mnamo majira ya kupukutika majani mwaka uliopita, Sam alikuwa na ji—jiwe ambalo hao wataalamu kule, kule—kule Tucson, walilichunguza. Lilikuwa kubwa kama marmar. Ndugu Sam Connelly . . . Wengi wenu hapa mnamjua; anatoka Ohio. Naye akaenda kwa daktari, akasema, "Sam, jitayarishe juma lijalo; nitalitoa hilo jiwe," siku chache baadaye.

Akasema, "Naweza kulitoa jiwe hilo kwa kujisaidia, daktari?"

Kasema, "Haiwezekani. Hilo jiwe ni kubwa mno."

76 Kwa hiyo akamwingiza kwenye gari akampeleka nyumbani. Naye akapiga simu; akasema, "Nataka uje uniombee, Ndugu Branham." Kwa nini akaniitia jambo kama hilo? Nami nikaanza kumwombea.

77 Nikasema, "Sam, ni BWANA ASEMA HIVI, hilo jiwe litatoka lenyewe."

78 Na asubuhi iliyofuata akalipeleka hilo jiwe kwa daktari. Naye akasema, huyo daktari akasema, “Bw. Connelly, sielewi ilivyotukia.”

79 Naye akasema, “Mimi ninamwamini Mungu, Naye Mungu aliniondolea jiwe hilo, alilitoa kwangu.” Ilikuwa vigumu kwa huyo mtu kuamini, huyo daktari. Kadiri tu asingaliweza kuamini juu ya ule uvimbe mkubwa kuondoka ubavuni mwa mke wangu. Mnajua habari hiyo, mnaona. Kwa hiyo akasema . . .

80 Yapata miezi sita baadaye, ambayo ilikuwa kama ninino tatu . . . kama majuma mawili yaliyopita, ama majuma matatu yaliyopita, Sam Connelly aliugua ugonjwa mbaya wa moyo. Nami sijui jina lake, mshipa wa damu moyoni, ama namna fulani ya kuziba moyo, ama cho chote kile. Ni hatari sana . . . Haitaninino . . . Huwezi kupona, wanavyodai. Ugonjwa mbaya wa moyo, na moyo wake ukaziba. Na viungo vyake vimevimba sana hata vifundo vyake vya miguu vilikuwa vikubwa kuliko mguu wake, hapa juu karibu na kiweo chake. Kwa hiyo wakamchukua wakampeleka kwa daktari. Daktari akasema, “Mchukueni mumpeleke nyumbani, kwa utulivu, ama hospitalini.”

Sam akasema, “Sitaki kwenda hospitalini!”

Kasema, “Mchukueni mumpeleke nyumbani mkamweke kitandani, na msimsogeze kichwa, mkono, ama mguu, kwa muda wa miezi sita.” Kasema, “Ungeweza kufa dakika yo yote.”

81 Ndipo Ndugu Norman akapiga simu. Nasi tukaenda kule usiku ule, kumwona Ndugu Sam. Na tulipomwombea, ndipo Bwana akanena.

Basi asubuhi iliyofuata, Sam akashuka akaenda kwenye afisi ya yule daktari, huku amekunja suruali yake, akasimama mbele ya daktari, akasema, “Nitazame, daktari!”

Ndipo daktari akamchunguza kwa mtambo wa stima wa kuchunguzia moyo, kisha akasema, “Sielewi jambo hili.” Kasema, “Rudi kazini.” Akasema, “Wewe ni wa kanisa gani?”

Akasema, “Mimi si mshiriki wa lo lote lile.”

82 Yeye akasema, “Huwezi kuwa Mkristo bila kuwa mshiriki wa hayo madhehebu. Huna budi kuwa mshiriki.” Mnaona, hayo tu ndiyo huyo daktari aliyojua. Sam alikuwa nati, kwake. Naye alikuwa nati, kwa Sam, kwa kuuliza swali kama hilo.

Ndipo nini kilitukia? Sam akaja, naye akasema, “Nimwambie nini mtu anayeniambia mambo kama hayo, Ndugu Branham?”

83 “Waambie ya kwamba wewe ni ‘mshiriki wa lile Kanisa moja la pekee.’ Hujiungi Nalo. Si madhehebu. Unazaliwa ndani Yake.”

84 Maskini bibi mmoja, yapata miezi sita iliyopita, huku anaegemea kifuani mwa Dada Norman. Nimesahau jina lake, mwanamke mrembo sana mwenye umri wa kama miaka thelathini. Yeye na mumewe walikuwa wameachana, naye akaugua ugonjwa wa leukemia. Naye alikuwa katika hali mbaya hivi kwamba ilikuwa vigumu kwake kutembea. Na hatimaye ikawa mbaya sana hata madaktari wakamlaza kitandani. Nao madaktari wakaenda kumwona hata wakati ukawadia. Wakampa hata Jumatano iliyofuata. Yeye atakuwa amekufa kabla ya Jumatano. Ndipo Bibi Norman kwa namna fulani akamtoa kitandani, akamleta huku, na ilimlazimu kumshikilia kwenye kiti. Na wakati maskini jamaa yule ameketi pale, akiyumbayumba huku na huko, na amepauka awezavyo kuwa; ngozi ya kimanjano, kutokana na hiyo kansa, leukemia.

Nikasema, "Vema, ninaweza kukuombea, dada."

Naye akijaribu kuzungumza, na machozi machoni mwake, akasema . . .

Ni—nikasema, "Wewe ni Mkristo?'

Akasema, "Mimi ni Mmethodisti."

Nikasema, "Ni—nilikuuliza kama ulikuwa Mkristo."

Naye akasema, "Unamaanisha kuwa mshirika wa kanisa la Kikristo?"

85 Nikasema, "La, mama. Ninamaanisha, wewe umezaliwa kwa Roho wa Mungu, na unampenda Bwana Yesu?"

Yeye akasema, "Vema, daima nimekuwa mshirika wa kanisa."

86 Nikasema, "Kama Mungu atakujalia kuishi, utaniahidi ya kwamba utarudi kwangu kusudi nikuonyeshe njia ya Bwana kwa udhahiri zaidi?"

Yeye akasema, "Namwahidi Mungu lo lote, iwapo atayahifadhi maisha yangu. Nitamtumikia."

87 Mara ono likaja, kasema, "BWANA ASEMA HIVI. Usijitayarishe; virarue vitu vya mauti yako, kesho kutwa." Hiyo ilikuwa Jumatatu, naye alikuwa afe Jumatano. "Hutakufa."

Jumapili iliyopita, Juma moja kutoka Jumapili hii, niliketi chumbani pamoja naye. Ameongezeka ratili thelathini na kitu; daktari alisema hakuna dalili yo yote ya leukemia ingeonekana mahali po pote. Naye alitaka kujua; nami nikampeleka ashuke aende akabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, katika mfereji wa kunyweshea maji shambani, njia ya Bwana. Huenda akawa nati, bali, "Nami nikiinuliwa juu, nitawavuta wote Kwangu."

88 Mimi hutembelea, kule kwa yule mvulana aliyekuwa anachukua kanda hapa, Leo Mercier. Yeye ana gari la kukokotwa. Nami nilikuwa nikiwaombea watu fulani. Nami nikamwombea maskini bibi mdogo jina lake Lokar, naamini

ndivyo alivyoitwa. Naye alikuwa amekwisha fanyiwa upasuaji mara kumi na nne wa kansa, nao madaktari wakamkatia tamaa afe. Naye akaombewa, na akaambiwa hatakufa, bali angeishi. Na hakuna dalili yake mahali po pote. Na kwa sababu ya tukio hilo, ishirini na nane wa jamii yake walikuwa wamesimama hapo, wameokoka na kujazwa na Roho Mtakatifu. Huenda likawa ni nati, bali linawavuta watu wote Kwake, ambao watakuja. Limeingizwa kwenye Neno. Mnaona ninalomaanisha?

89 Nina barua iliyokuja, majuzi, imewekwa kule nyuma katika faili. Mnamo majira ya Kupukutika Majani mwaka jana, nilipokuwa mawindoni . . . ama, kwenye msimu wa Kuchanua Majani, ilikuwa mwaka mmoja uliopita. Mvulana wa Kihindi anayeitwa Oscar, ambaye tunawinda naye kwenye barabara kuu kule; ilikuwa mahali ambapo Malaika wa Bwana, niliwaambia, kupitia hapa, angemleta yule kulungu dume na—na yule dubu mkali mwenye kichwa cha rangi ya fedha. Nyote mnakumbuka jambo hilo. Ndipo huyo mvulana, nilipotembea nikaingia . . . Yeye akaingia hemani, kwenye majira yaliyopita ya Kuchanua Majani. Basi Budd aliponiomba kuomba dua, (yeye alitoa glavu zake; alikuwa anapanda farasi), akazivaa hizo glavu na alikuwa tayari kwenda zake. Alikuwa Mkatoliki. Hakutaka kuhusiana na Kitu hicho.

90 Kwenye majira yaliyopita ya Kupukutika Majani, wakati alipoweza, huku amesimama karibu yangu . . . Mama yake alipokuwa kule nyuma, anakufa kwa ugonjwa mbaya wa moyo, alisema, “Je! utarudi kuja kumwombea?” Nilirudi katika kile kibanda cha Wahindi pale. Na hapo, hao wote wamekusanyika wakimzunguka huyu mama, naye yuafa, asingeweza kuzungumza hata neno moja la Kiingereza. Naye Roho Mtakatifu akashuka akamwambia huyo mama, kupitia kwa mkalimani, bintiye, yale yaliyokuwa yametokea, ambayo yalikuwa. Hata alimwita jina lake, na kumwambia alikuwa nani, na alitoka kwenye kabila gani, na jinsi ambavyo jambo hili lingetukia. Naye huyo mama aliponywa papo hapo.

91 Basi asubuhi yake niliporudi kuwaona, nilipokuwa ninaondoka kwa farasi, nikirudi maili arobaini kwa ajili ya kondoo mmoja, hao hapo wote wameketi pale, yule mama alikuwa . . . alikuwa anapanda farasi arudi akale nyama kavu za kongoni. Nami nikasema, “Jana usiku nilipoomba, nilisema, ‘Baba yetu aliye Mbinguni.” Nikasema, “Louise, ni—ni . . . Ilikuwa sala ya Kikatoliki. Nyote mlianza, halafu, bila shaka, nikawaacha.” Kisha nikasema, “Sasa nitamshukuru Mungu. Sisi hatukariri maombi; sisi huomba.”

92 Mama akasema, “Sisi si Katoliki tena.” Akasema, “Sisi tunaamini jinsi unavyoamini. Tunataka utuchukue sisi sote ukatubatize jinsi wewe unavyobatiza. Tunamtaka Roho Mtakatifu.”

93 Katika safari ya kurudi. . . Yule mvulana alikuwa amewapoteza farasi wake, miezi kadha kabla ya tukio hilo, hangeweza kuwapata. Naye yule kiongozi alikuwa akimkemea sana, kasema, "Oscar, ulijua vizuri zaidi kuliko kuwaacha hao farasi namna hiyo. Hao dubu, wengi wakali sana wangewala hao farasi kufikia wakati huu."

Naye akaendelea kusimama karibu yangu. Kisha akasema, usiku mmoja, yeye akasema, "Mimi nikuulize kitu fulani?"

Nikasema, "Naam."

Kasema, "Ndugu Branham, omba Mungu. Mungu nirudishie farasi wangu."

Nikasema, "Bud alisema dubu wamewala."

Kasema, "Ndugu Branham, omba Mungu. Mungu amrudishie Oscar farasi wake."

Nikasema, "Unaamini hivyo, Oscar?"

Yeye akasema, "Naamini. Mungu mfanya mama yangu mzima. Mungu kwambia mahali dubu alikuwa, mahali wanyama walikuwa. Mungu huyo, jua mahali walipo wanyama, jua mahali walipo farasi wangu." Mnaona?

94 Mwaka mmoja uliopita, nilipokuwa nimesimama kule nyuma na Fed Sothmann, ambaye yuko hapa usiku wa leo, Billy Paul, mwanangu. Roho Mtakatifu alishuka. Nikasema, "Oscar, utawapata farasi wako. Watakuwa wamesimama kwenye barafu."

Barua iko hapa, niliyoandikiwa juma lililopita, nami nikaipata Ijumaa, nikaja huku. Iko pale kwenye faili sasa. "Ndugu Branham, Oscar kapata farasi wamesimama katika theluji."

95 Jinsi walivyoishi, hakuna ajuaye. Hapo, yule mvulana. . . Wakati kama huu mwakani, Juni, kuna theluji nyingi sana kungali kuna futi ishirini za theluji zimewazunguka. Walikaaje kule majira yote ya kipupwe, katika magenge haya? Oscar anaweza kuwafikia, huku amevalia viatu vya theluji, lakini, bila shaka, yeye hawezi kuwavalisha hao farasi wake viatu vya theluji. Bali aliwapata, kulingana na Neno la Bwana. Huenda jambo hilo likasikika kama nati; liamini tu wakati mmoja! Inategemea jinsi hesi zako zilivyo.

96 Sasa, halitaingiana na madhehebu. Litaingiana tu na Neno. Bali kuna watu katika ulimwengu huu wanaoamini hilo Neno! Itahitaji nati kumfunga huyo Bibi-arusi atoke hapa, bila shaka, kwa maana Bibi-arusi na Bwana arusi ni mmoja. Na huyo Mungu ni mmoja, nalo Neno ni Mungu! Itapaswa kuingizwa kwenye Neno, nalo litamvuta Bibi-arusi atoke katika madhehebu haya.

97 Naam, yeye alitaka kunitoa makosa. Mnajua, inanikumbusha juu ya kuzungumza, asubuhi hii, juu ya Mungu akijificha nyuma ya ngozi, ngozi ya mwanadamu.

98 Hadithi ndogo, kisha nitafunga; nasikitika kwamba niliwaweka hapa kwa kama dakika arobaini na tano sasa. Kuna nyumba fulani, nyumba ya Kikristo, na kulikuwa na . . . Nilimsimulia haya yule mtoa lawama. Na katika nyumba hii kulikuwa na . . . Wao walimwamini Mungu. Walikuwa na mvulana mdogo pale, bali alikuwa anaogopa sana dhoruba. Radi, loo, aliogopa mno. Yeye angekimbia aingie chini ya meza, po pote pale, radi ikija.

Kwa hiyo usiku mmoja dhoruba kubwa sana ikatokea kule shambani, na mahali walipoishi, na miti ilikuwa inavuma, na radi inamemetesha, huku inazidi kuwa giza. Mama akamwambia Kadogoo, kasema, “Sasa, Kadogoo, nenda kwenye chumba cha juu ukalale.” Kasema, “Basi, usiogope. Panda uende kule.”

99 Kwa hiyo maskini Kadogoo, akiwa na nguo zake za kulala, akapanda akaenda kwenye chumba cha juu, akiangalia nyuma, nusu akilia. Akalala, akajaribu kulala usingizi, akafunika kichwa chake. Hangeweza kulala; hiyo ikimemetesha dirishani. Kwa hiyo yeye akasema, “Loo, mama,” kasema, “njoo hapa ukalale nami.”

Vema, yeye akasema, “Kadogoo, hakuna kitu kitakachokusumbua. Radi hiyo haiwezi kukudhuru.”

Akasema, “Lakini, mama, njoo huku ukalale nami.”

100 Kwa hiyo huyo mama akapanda kwenye vipandio akajilaza kitandani, pamoja na Kadogoo wake. Naye akasema, “Kadogoo, mwanangu mdogo, mama anataka kukwambia jambo fulani.” Akasema, “Kadogo, sisi ni jamaa ya Kikristo. Tunamwamini Mungu, nasi tunaamini ya kwamba Mungu hutulinda katika dhoruba. Tunaamini jambo hilo. Pia tunaamini ya kwamba Mungu huwalinda walio Wake.” Kisha akasema, “Nataka uamini jambo hilo, Kadogoo. Ya kwamba, usiogope. Mungu yu pamoja nasi, Naye atatulinda.”

101 Kadogoo akapuuza mara chache. Akasema, “Mama, ninaamini jambo hilo, pia. “Akasema, “Bali wakati radi hiyo iko karibu sana na dirisha, nataka kuhisi Mungu aliye na ngozi.”

Kwa hiyo nafikiri wengi wetu sisi watu wazima tunafikiria vivyo hivyo. Mungu, aliye na ngozi! Linaweza likasikika kama nati, kwa ulimwengu, bali linawavuta watu wote Kwake.

Na tuombe.

102 Baba wa mbinguni, kama hadithi ndogo za—za matukio, na wakati mwingine zinatendeka kwa sababu fulani. Na ni, na hata iwe fidhuli jinsi gani, hata hiyvo tunalifahamu katika lugha liliyotendeka. Kwa hiyo tunakushukuru, usiku wa leo, Bwana, ya kwamba—ya kwamba Mungu anaweza kujifanyia makao ndani yetu. Tunashukuru ya kwamba kulifanywa upatanisho, Damu ya Mwenye haki, Yesu: Ambaye alikuwa ukamilifu wa Mungu,

ukamilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili, ya kwamba aliyatoa maisha yake ya thamani; hayakutolewa Kwake, bali aliyatoa kwa hiari, ili kwamba tupate kufurahi katika ukamilifu wa Uwepo Wake, katika utukufu wa Shekina alimoishi; ili kwamba nafsi zetu zitakaswe na Damu hiyo, ili kwamba Roho Mtakatifu aliye mkuu apate kuishi ndani yetu. Nasi tunakuwa waalimu, manabii, na kadhalika, kwa hao watu, kwa hao, Bwana, walio wahitaji; karama za Mungu; Mungu Mwenyewe akidhihirisha, aking'arisha karama kuu za Mungu, mbele ya huu wakati wa kisasa.

103 Na tamshi hili fidhuli, Bwana, la kuwa nati. Nasi tunajua, ya kwamba katika siku hii, ya kwamba inachukua wakati mwingine wakati ulimwengu uko katika taratibu kama vile kanisa lilivyo leo, kujiunga tu na makanisa mapya na madhehebu mapya. Mtu anayejitokeza na Neno hudhaniwa kuwa nati, mtu mwenye kichaa. Kama yule mtume maarufu Paulo, ambaye alifunzwa kuwa mwanathelojia, kuhani, na hata hivyo alisema kwamba alifanyika mjinga, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Aliacha elimu yake, ili kwamba watu wapate. . . kusikiza maneno yake yenye ufasaha. Naye alisema alikuja si kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, ili kwamba imani yao iwe katika vitu kama hivyo. Jinsi kanisa limegeukia mambo hayo leo, kama alivyotabiri, "Baada ya kuondoka kwangu, mbwa mwitu wataingia, wasilihurumie kundi." Bali yeye alisema alikuja kwao, "katika nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu," kusudi imani yao iwe katika Mungu. Baba, yeye alifanyika mjinga, kwa ulimwengu, apate kumjua Yesu.

104 Na ndivyo tufanyavyo leo, Bwana. Kuna watu wanaoketi hapa ambao wanadhaniwa ni wenye kichaa, kwa sababu wako tayari kumtumaini Mungu kwa ajili ya kuponywa kwao, kwa ajili ya kikomo chao cha Milele. Wakihatarisha sifa zao, kwa kumwabudu Yeye. Wakimshukuru Yeye, wakimsifu Yeye, wakizipa roho zao uhuru, kumwabudu Mungu; wanadhaniwa kuwa ni wenye kichaa. Bali Wewe ulisema, ya kwamba, "U— upumbavu wa Mungu," kama sisi ni wajinga, "ulikuwa na nguvu na hekima zaidi ya hekima ya mwanadamu; kwa kuwa mwanadamu, kwa hekima, hakumjua Mungu. Bali kwa upuzi wa kuhubiri, ilimpendeza Mungu kuwaokoa wale waliokuwa wanaweza kuokolewa." Tunaomba, Mungu, ya kwamba yule Mwandishi mkuu wa Neno hili atakuja usiku huu na kuwaponya wagonjwa, kuwaokoa waliopotea. Tunaomba hilo katika Jina la Yesu. Amina.

105 Ninamfananisha Mungu, kusudi msitatanishwe na yale niliyosema leo; Mungu ni Almasi iliyo kuu, ya Milele.

Na wakati almasi inapotolewa kwenye jiwe samawati la Afrika, nimekuwa kwenye ile migodi na kuyaangalia kwenye ninino kuu. . . jinsi wanavyoyatengeneza haya na kuitoa almasi,

jinsi yanavyopitia kwenye mtambo wa kuyavunjia, na ule moto mkuu wa samawati wa almasi, almasi nyeusi zinatoka. Hazina umbo sana, umbo maalum. Hizo ni mawe makuu tu. Na, kwa kweli, hayana moto ndani yao wakati huo. Hayo ni almasi tu, jiwe; mviringo, laini, mengi sana. Bali almasi hii haina budi kukatwa. Naam, si halali kuwa na moja isiyokatwa. Haina budi kukatwa, ndipo huna budi kuwa na risiti ya mahali ulipoinunua, kwa maana zina gharama ya mamilioni ya dola.

Nami ninamfananisha Mungu na almasi hiyo.

106 Sasa, almasi inakatwa kusudi ipate kurudisha mng'ao wa kile kilicho ndani yake, ule moto ulio katika almasi. Na haina budi kukatwa kwa kila njia ndogo, kila sura ndogo, ncha tatu. Weka ncha tatu kwa almasi, na nuru ikielekezwa kwa kitu kilicho na ncha tatu kitatoa rangi saba, mnaona, kitatoa rangi saba.

107 Na sasa angalia, "Mungu alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu." Mnaona, Yeye alikatwa, akachubuliwa, huyo Almasi mkuu, kusudi kutoka Kwake karama zidhirishwe kanisani.

Na si ile nuru; kwa sababu, ile nuru haina budi kurudi, wakati jua limeondoka kwake, mahali ilipotolewa.

Lakini kila kipande kidogo kinachotoka katika vipande hivyo vidogo hakiharibiwi; kinatumiwa. Vingi vya hivyo hutumiwa katika sindano za Santuri. Na hizo sindano zinatoa, ambazo zimekatwa kutoka kwa almasi, zinatoa muziki ambao umetiwa kwenye sahani ya santuri.

108 Nami natumaini mtaona kile ninachomaanisha. Kile kipande kilichotolewa kwa Kristo, kile kipawa toka kwa Kristo, kikawekwa katika Biblia, kinanena kwa mwamini siri za Mungu zilizofichwa. Yeye anajua siri ya moyo. Yeye anamjua kila mtu. Mnaamini hayo?

Haingekuwa almasi ikisema, "Mnaona nilivyo mimi?" Ni kile ilichotoka kwake. Almasi ni almasi kwa sababu imetoka kwa almasi.

109 Na hivyo ndivyo zilivyo karama za Roho, kwa huyo mtu, ni sehemu ya hiyo Almasi. Imetumwa, na imeshushwa, na kuletwa katika kipawa, kufasiri, kuhubiri, kufundisha. Kuna karama tano za kiroho; mitume, manabii, waalimu, wachungaji, wainjilisti, na zote ni za kuujenga Mwili wa Kristo. Na kwa uhakika kama kulivyo na waalimu, wachungaji, hapana budi kuwe na manabii. Tunajua hivyo.

110 Nasi tunaamini ya kwamba Mungu hana budi kudhihirishwa katika siku za mwisho, miongoni mwa watu Wake, kwa Mzao ulioteuliwa, kulingana na Biblia, katika mfano wa nabii. Hiyo inalingana kabisa na Neno. Si kwamba huyo mtu ni Mungu, bali hiyo karama ni Mungu. Mnaona? Na hiyo ndiyo ile sindano.

Naam, pini haitacheza hiyo sahani ya santuri vizuri. Sindano ya kawaida ya kushona haitaicheza vizuri. Lakini almasi, ndiyo bora zaidi. Inatoa sauti nzuri, sindano yenye ncha ya almasi.

111 Naomba kwamba Mungu, usiku huu . . . Taarifa yako ya maisha, hata uwe na kasoro gani, cho chote unachotaka kutoka kwa Mungu, naomba kwamba yule Bwana mkuu Ambaye anashikilia ile sindano mkononi Mwake, na aiweke maishani mwako na atufunulie kile kilichokuleta hapa, unachohitaji; ndipo tutajua ya kwamba Yeye yuko hapa.

112 Baba wa mbinguni, naomba utukirimie hilo kabla sijaanza mstari huu wa maombi, sikusudii kufanya hivi, bali naomba kwamba ufanye hivyo, ili kwamba watu wapate kujua. Labda wageni wako hapa kuombewa. Siwajui, bali Wewe unawajua. Naye Paulo alisema, "Kama ukinena kwa lugha, na kusiwe na kufasiriwa ama haijengi, watu watasema ninyi ni wenda wazimu. Bali kama mtu akitoa unabii na kufunua yaliyo katika moyo, basi wao watasema, 'Kweli Mungu yuko pamoja nanyi.'" Na iwe hivyo tena, Mungu, katika wakati huu uliochelewa sana. Wewe uliahidi jambo hilo, na ndivyo litakavyokuwa. Katika jina la Yesu Kristo. Amina.

113 Sasa sijui ni watu wangapi walio wagonjwa hapa usiku huu, walio hapa? Ama je, Billy alisambaza . . . za maombi? Kuna kadi za maombi zilizotolewa? [Ndugu wanasema, "Ndiyo."—Mh.] Ziko. Vema, nadhani kila mgonjwa ana kadi ya maombi, bali sijui ulichoandika ndani yake. Nafikiri yeye huwapa tu kadi; unaandika lo lote unalotaka juu yake. Sivyo? Ulipata tu kadi; ukaandika ndani yake lo lote unalotaka.

114 Sikujui. Ni wangapi hapa wanajua siwajui, na hata hivyo mu wagonjwa, nawe ungesema hivi, "Yale nimekusikia ukisema leo, 'Mungu nyuma ya ngozi. Mungu nyuma ya ngozi ya mwanadamu, akijitia utaji'"? Bali kama una macho ya kiroho, ungeyafungua na kumwona Yeye, uone Yeye ni Nani. Nawe uamini jambo hilo. Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya; nyingi kuliko hizi atazifanya, kwa maana naenda kwa Baba." Sasa, kama unaamini kwa moyo wako wote!

115 Ni wangapi hapa ndani walio wagonjwa, na wanajua ya kwamba siwajui, sijui mna kasoro gani? Inua tu mkono wako, useme, "Mimi ni mgonjwa. Nina haja." Ni wangapi walio na haja moyoni mwao, si wagonjwa, bali wana haja? Mnajua mnazihitaji . . . Sawa. Hakuna mtu ye yote pale, ambaye ninamwona, ila aliyeuinua mkono wake. Naam, sijui . . .

116 Ninamjua mtu huyu anayeketi hapa. Nina hakika huyo ni Ndugu James, na nafikiri huyo ni Dada James. Ndugu Ben, najua. Nyuso zenu tu, wakati mwingine; huyo ndugu anayewapiga picha. Bali ile . . .

Hebu mtu fulani nyuma humu, mahali po pote, ninino tu . . . Na—na—nasai jambo hili, juu ya msingi, na kumalizika kwa Ujumbe huu.

117 Unajua Mungu aliahidi jambo hili kutukia katika siku za mwisho? Yeye alifanya ahadi. Mnaona? Sasa siwezi kulifanya litukie. Mnaona, si—siwezi kufanya hivyo. Yeye hana budi kufanya jambo hilo. Yeye ndiye anayefanya jambo hilo; si mimi. Bali mimi ninamwamini Yeye, la sivyo nisingekuwa nimesimama hapa nikiwaambia jambo ambalo sikuliamini. Sasa, ninyi ombeni, na mseme, "Bwana Yesu, nimefundishwa katika Biblia ya kwamba Wewe ni Kuhani Mkuu sasa hivi, ambaye anaweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu." Sijali uko wapi. Nawe sema tu, "Ninakuamini. Na, kwa imani, ninaamini yale yule mtu aliyosema leo."

118 Hivyo ndivyo yule Malaika alivyoniambia, "Wafanye watu wakuamini." Na kama nikiwahubiri Neno la Mungu, si ati "niaminini mimi," ni "aminini Neno."

Kama haliambatani na Neno, basi usiliamini. Bali kama unaamini ni Neno, basi, hata liwe nini, wewe omba na uamini, na uone kama Yeye yungali anaweza kufunua yale yaliyo ndani ya moyo wako.

119 Na mtu ye yote anajua ya kwamba Biblia ilisema, ya kwamba, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, na hutambua mawazo na makusudi ya moyo."

Hivyo ndivyo Ibrahimu alivyojua ya kwamba huyo alikuwa ni Mungu, wakati angaliweza kujua yale Sara alikuwa anasema huko nyuma hemani, yale aliyokuwa anawazia; wakati aliposema, "Nitakuzuru," naye Sara akawaza moyoni mwake, "Haiwezekani."

120 Sasa, nilisema Yeye yuko hapa kukuponya. Unafikiri nini juu ya jambo hilo? Kama tu utaamini! Sasa, siwezi, sina njia yo yote; Mungu wa Mbinguni anajua jambo hilo. Mnaona? Sina budi kuliona. Na ninaloona, nalisema; na lile ni—nisiloona, bila shaka, siwezi kulisema. Bali Yeye yungali Mungu vile vile! Je! jambo hilo lingeiongeza imani yako, kama angefanya hivyo?

Nikihubiri namna hiyo, kwa namna fulani inanitupa nje kidogo. Bali Yeye yuko hapa. Ninahisi jambo hilo. [Ndugu Branham anatulia—Mh.]

121 Nikimtazama mtu alipokuwa anaimamisha kichwa chake, papa *hapa* nyuma. Mke wake anaketi karibu naye, akiomba, pia. Papa *hapa*. Una kitu moyoni mwako. Mkeo, anaomba. Una mzigo moyoni mwako. Ni wa mama mkwe wako. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia mama mkwe wako ana kasoro gani? Sikujui. Sisi ni wageni mmoja kwa mwingine. Kwa hiyo hiyo ni kweli? Unaamini Mungu anaweza kuniambia ana kasoro gani? Yeye hayuko hapa. Ninaona mahali palipo mbali; yeye yuko mashariki ya hapa. Yeye yuko Ohio. Hiyo ni kweli.

Yeye anaugua ugonjwa wa damu. Hebu mke wako ampelekee hiyo leso pale, ambayo analilia, aiweke juu yake. Usitie shaka; yeye atapata afya. Unaamini jambo hilo?

122 Hapa kuna bibi mdogo anayeketi papa hapa mbele yangu. Analia. Mtoto huyo ana kasoro, sijui . . . La, hana kasoro. Yeye ana shauku tu. Ana shauku ya kumpokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Amini, ewe mtoto, utampokea. Hiyo ni kweli. Usitie shaka.

123 Hapa yupo bibi anayeketi hapa kwenye mwisho wa safu. Yeye anaomba. Mimi ni mgeni kwake, bali ana kivuli. Ulikuwa umefanyiwa upasuaji mara nyingi. Kama sisi ni wageni mmoja kwa mwingine, nafikiri. Sikujui. Wewe hunijui, labda ni kwa kunisikia tu. Wewe hutoki hapa. Wewe ni mgeni kati yetu. Umetoka Wisconsin. Mji huo ni Milwaukee. Na shida yako ni kansa; iko kwenye titi. Upasuaji baada ya upasuaji, hata hivyo bila ya kufanikiwa. Hebu imani ile, iliyougusa upindo wa nguo Yake, iamini hiyo sasa hivi. Ididimize moyoni mwako; itatimia. Uwe na imani!

124 Mtu fulani anayeketi pembeni hapa. Yeye anamwombea mama yake. Yeye ni mgeni kwangu. Simjui. Bali yeye anamwombea mama yake. Na mamaye ana kitu kile kile alicho nacho mwanamke huyu, kansa. Ama, yeye anaiogopa, na ndivyo ilivyo. Kuna mtu unayemwombea, na mtu huyo ana shida ya mgongo wake. Yeye, pia, namwona amelewa sana. Yeye ni mlevi wa kupindukia. Ndugu yako. Wewe hutoki hapa. Umetoka Illinois. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia jina lako ni nani? Farmer. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako. Amininі!

125 Kuna mtu anayepiga magoti juu ya mtu fulani, akiomba, mtu ambaye amelala kwenye machela. Sawa. Unaamini yale umesikia, kuwa ni Kweli, bibi? Unaamini. Kama ningaliweza kukuponya, ningekuja na kufanya hivyo. Bali tayari umekwishaponywa na Kristo, unaona. Inakubidi tu kuamini jambo hilo. Huyo bibi anayesimama hapo, akiomba, alikuwa akikuombea uguswe. Sikujui, bali Mungu anakujua. Umetoka nje ya mji, pia. Hiyo ni kweli. Umetoka Illinois. Hiyo ni kweli kabisa. Jiji hilo linaitwa East Moline, Illinois. [Yule dada anasema, "Hilo ni jiji nilimozaliwa."—Mh.] Unaugua kansa. Wewe ni mke wa mhudumu. Unaamini? ["Naam."] Utakufa, ukilala pale. Mbona usimkubali usiku huu, na useme, "Naweza, moyoni mwangu, huku imani yangu ikiwa juu ya kila kitu kilicho hapa, ninaamini ya kwamba nimeponywa. Niko katika Uwepo wa Mungu." Inuka, amini, na uende nyumbani ukaponywe. Huyo hapo.

Mnaamini kwa mioyo yenu yote? [Kusanyiko linafurahi—Mh.] Na tumsifu Mungu.

126 Baba wa Mbinguni, tunakushukuru kwa wema Wako wote na rehema Zako. Tunakushukuru, kwa kuwa, Wewe ungali hapa,

katikati kabisa ya shida hizi zote. Katika ulimwengu huu ambao umepotoka, hata hivyo Wewe uko hapa. Naomba kwamba Roho Wako, Bwana, adumu pamoja nasi daima. Tunaona ya kwamba uko hapa, Mungu aliyejivika ngozi, katika mioyo ya binadamu; ukitoa imani, na ufunuo, na ono. Wewe ni Mungu katika Kanisa Lako, Mungu katika watu Wako. Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili, Bwana. Na naomba kwamba kila mmoja aamini, usiku huu, kwa moyo mmoja, na jalia kwamba waponywe. Kwa Jina la Yesu Kristo, naomba. Amina.

127 Ni wangapi upande huu walio na kadi za maombi, upande *ule*? Hebu hao walio upande *ule*, warudi nyuma, waje moja kwa moja katikati ya marefu haya. Hao walio kwenye *yale* marefu, waje moja kwa moja upande *huu*, chukueni mahali penu tu, njoni moja kwa moja upande *huu*. Hebu hao, mara watakapokuwa wamekwisha, mstari huu ushikamane na ule mwingine.

128 Wazee wa kanisa waje hapa. Ndugu Roy, Mungu akubariki; sikujua ulikuwa umeketi hapo. Nawataka mashemasi wa kanisa hapa mara moja, kama wanaweza kuingia kutoka po pote walipo. Njoni mkasaidie kidogo.

Namtaka kila mtu atakayeombewa, inua mkono wako, useme haya nyuma yangu.

Bwana, [Kusanyiko, "Bwana,"—Mh.] Naamini. ["Naamini."] Nisaidie kutokuamini kwangu. ["Nisaidie kutokuamini kwangu."] Naamini ["Naamini"] ya kwamba katika Uwepo Wako, ["ya kwamba katika Uwepo Wako,"] ninapolifuata Neno Lako, ["ninapolifuata Neno Lako,"] na ninino yangu . . . nimewekelewa mikono usiku wa leo, ["na nimewekelewa mikono usiku wa leo,"] nitakubali kuponywa kwangu, ["nitakubali kuponywa kwangu,"] katika Jina la Yesu. ["katika Jina la Yesu."] Amina. ["Amina."] Mungu awabariki.

129 Sasa angalia. "Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Yeye alimwambia Nuhu itanyesha. Haikunyesha—Yeye kamwe . . . Mimi sikusema kamwe, "Mara tu—mara tu utakapoombewa, utakuwa mzima." Alisema, "Watapata afya."

130 Yeye alimwambia Nuhu itanyesha. Haikunyesha kwa miaka mia moja na ishirini, bali ilinyesha.

Alimwambia Ibrahimu atampata mtoto kwa Sara. Haikutendeka kwa miaka ishirini na mitano, bali alimpata.

Alimwambia Isaya bikira atapata mimba. Haikutukia kwa miaka mia nane, bali akapata mimba.

Sivyo? Yeye aliahidi hilo! Haidhuru ichukue muda gani, Yeye hufanya hivyo, kwa vyo vyote. Ninyi aminini hilo.

131 Njoni mbele sasa. Hebu Ndugu Capps aongoze nyimbo. Utaondoa kadi? Sasa hebu kila mtu awe katika maombi sasa.

132 Baba yetu aliye Mbinguni, tutazitii amri Zako kwa kuwawekea mikono hawa wagonjwa. Sijui jambo jingine moja ambalo Wewe ungefanya, Bwana, kwa kuwa umesema, katika Neno Lako, umenunua kuponywa kwao. Umethibitisha ya kwamba uko hapa pamoja nasi usiku wa leo, Neno ambalo linaweza kuyatambua mawazo yaliyo moyoni. Umethibitisha jambo hilo, ya kwamba Wewe uko miongoni mwetu. Nami nakuomba, Wewe, Baba, ya kwamba Neno Lako, ambalo haliwezi kushindwa, litafanywa halisi sana kwa kila moyo! Ambalo ulisema, "Kama mnaweza kuliamini; msitie shaka, bali mliamini; muuambie mlima huu, 'Ng'oka,' na msitie shaka, bali muamini kwamba itatimia!" Yeye hakusema ni lini.

133 Wewe uliwaambia wale watu, kwenye Pentekoste, wapande waende kule wakangoje. Wewe hukusema kamwe masaa, siku; ulisema, "hata." Sasa wao wanakuja kukubali kuponywa kwao. Naomba wasifikirie lingine ila kuponywa kwao, hata ukombozi wao utakapokuja. Tunakutii Wewe kwa kuwawekelea mikono, kama waamini. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

134 Vema, njoni mara moja. [Ndugu Branham na hao ndugu wanawawekea watu hao mikono, na kumwombea kila mmoja kwenye mstari wa maombi. Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] Mmeponywa. Mungu awabariki. Hilo ni zuri. [Mahali patupu kwenye kanda.]

> Yote yatendeka, amini tu;
> Amini tu, amini tu,
> Yote . . .

Bwana Yesu, naziombea leso hizi sasa, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Sijui kama tungeweza kuyabadilisha maneno hayo:

> Sasa naamini, sasa naamini,
> Yote yatendeka, sasa naamini;
> Sasa naamini, sasa naamini,
> Yote yatendeka, sasa naamini.

135 Unaamini ya kwamba yaliyoombwa na kutakwa yatatolewa? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Yatatukia.

136 Niliona, nilipokuwa napita mstarini muda mchache uliopita, baadhi ya marafiki wangu Waitaliano kutoka Chicago. Ni wangapi wanamjua Dada Bottazi kutoka Chicago? Vema, mnajua, yeye alikuwa na ugonjwa wa bo—bongo, ugonjwa wa kufadhaika akili hivi majuzi, mbaya sana, sana. Lakini asubuhi huko Chicago kwenye kifungua kinywa cha Wafanyi Biashara Wakristo, nilimwambia huyo dada, chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu. Alirudi upande mmoja, naye hangeweza kujimudu. Ndipo nikasema, "Dada, wewe hutapata afya mara moja, bali utapata afya." Nikasema, "Itakuwa aidha miezi kumi na minane, ama miaka miwili, papo hapo kwenye kipindi hicho utaponywa."

137 Juzijuzi nilipokuwa nikizungumza naye. . . Nilimsikia akishuhudia, akiwa na furaha sana, mwenye furaha sana kuliko alivyowahi kuwa maishani mwake mwote. Alikuwa anaendesha motokaa. Hakuwa na amani, Uwepo wa Mungu ulionekana kana kwamba umemwacha; bila shaka, ilikuwa neva ya ubongo, mwajua; mara ukarudi na mbubujiko mkubwa wa furaha, na nguvu za Roho Mtakatifu zilikuwa juu yake. Akalia, akapaza sauti, a—alikuwa. . . Walikuwa tu na wakati mzuri sana, yapata majuma matatu manne yaliyopita, ama mwezi mmoja. Nami nikamsikia akishuhudia, Jumapili iliyotangulia iliyopita, naye akasema, "Ndugu Branham, niliporudi, niliandika na kuchukua kanda ile. Na ilikuwa miezi kumi na minane hasa, siku ile ile." Amina.

Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Si Yeye ni wa ajabu? ["Amina."]

138 Naam, Roho Mtakatifu yeye yule anayeweza kubashiri kwa usahihi sana, bila kukosea hata wakati mmoja, miaka hii yote; na, kupitia kwa Neno Lake, amejaribu kuwafunulia ninyi leo ya kwamba Mungu si kitu fulani kilicho mbali mahali fulani ama kitu fulani cha kihistoria. Yeye ni Neno lililodhihirishwa, lililo hai na la wakati uliopo. Alijificha Mwenyewe katika utaji wa binadamu, katika Kanisa Lake, akijifunua Mwenyewe kwa imani yako na imani yangu, pamoja, kutuunganisha pamoja, tukifanya umoja wa Mungu. Mimi siwezi kufanya kitu bila ninyi; ninyi hamwezi kufanya kitu bila mimi; hakuna anayeweza kufanya kitu bila Mungu. Kwa hiyo, sote pamoja linafanya kitu kimoja, ule muungano. Mungu alinituma kwa kusudi hilo; mnaamini jambo hilo; na hapa linatendeka. Ndilo hilo hasa, mnaona, limehakikishwa kikamilifu.

Sijali una kasoro gani, yale aliyosema mtu ye yote; kama, kutoka moyoni mwako, unaamini ya kwamba utapona, hakuna kitu kinachoweza kukuzuia. Yeye alisema hivyo. Pia alisema, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa." Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

139 Ni wangapi watakaoniombea katika mikutano mingine nitakapokwenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mimi ndimi ninayehitaji maombi. Mnaona? Kila mtu amenikataa, mnaona, ila ninyi, na hata hivyo kuna Mzao kule nje.

140 Nilituma barua kule Afrika Kusini. Wasingeniruhusu kuingia isipokuwa kama ningetia sahihi karatasi ya kwamba mimi "ningebatiza, huko upande mwingine, kila mtu mara tatu; mara moja kwa Baba, na mara moja kwa Mwana, na Roho Mtakatifu, kifudifudi. Upande mwingine, ningebatiza kichalichali, mara moja kwa Baba. . . Na kufundisha hilo ndilo Fundisho."

Nikawaandikia barua. Nikasema, "Roho Mtakatifu amekuwa akijaribu, kwa miaka michache iliyopita, kunipeleka

Afrika tena. Yeye anataka kuitumia huduma yangu kule mahali ambapo elfu thelathini walimkubali Kristo alasiri moja." Nikasema, "Kumbukeni, damu ya watu hao na iwe juu yenu, si juu yangu. Nimejitolea kuja, bali hamtafanya jambo hilo."

Sijui itakuwa namna gani kwenye siku hii ambayo Yesu, Mwana wa Mungu amekataliwa na kanisa, Neno limekataliwa? Bali katika—katika yote hayo, Yeye angali bado anajijulisha Mwenyewe kwa watu Wake. Je! hamna shukrani kwa jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

141 Nami nilipita, usiku wa leo, nikawawekelea mikono yangu, baadhi ya wanawake wazee, wengine vijana, wengine wazee, wengine vijana wanaume, wanaume wazee, wamelowa kama nilivyo mimi. Nikawaza, "Wameketi pale, wameketi pale wakilisikiliza Neno ambalo ulimwengu wa nje unadhani ni wazimu." Mnaona? Wao ni—wao ni skrubu. Mnaona, Mungu yuko hapa kuitia hesi, akuvute akutoe moja kwa moja kutoka kwenye magonjwa yako. Ni ahadi ya Neno. Kumbukeni tu, itaanza kukaza, "Nitawavuta; kama nikiinuliwa juu, nitawavuta." Ataivuta aitoe kwako. Bila shaka ataivuta. Wewe mwamini tu, uwe na imani Kwake. Usimtilie shaka. Mwamini.

142 Niombeeni. Wakati hamna mtu mwingine wa kuombea, nikumbukeni tu!

> Halafu hata twonane huko juu! hata twonane
> Kwake kwema!
> Hata twonane . . .

Asanteni kwa kuja kutoka mbali namna hiyo. Mungu na awalinde mnapoondoka kwenda nyumbani!

> Hata two- . . .

Wasalimuni Wakristo wote, waamkueni, kutoka kwenye kundi hili hapa. Amani ya Mungu iwe pamoja nanyi! Shalom!

> Mungu awe nanyi daima!
>
> [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Mungu Awe Nanyi*—Mh.] . . . huko juu!
>
> Hata twonane Kwake kwema;
> Hata twonane huko juu!
> Mungu awe nanyi daima!

143 Nina furaha sana. Mnaona, kuna mengine, mambo mengi nisiyojua, bali yapo mengine ninayojua. Ninashukuru sana kwa ajili yenu. Nina furaha sana kushirikiana pamoja nanyi. Nina furaha sana kuwa mmoja wenu. Mungu awe nanyi.Atakuwa nanyi. Yeye hatawaacha kamwe. Hatawapungukia. Yeye hatawaacha. Tayari mmekwisha pita katika ile pazia. Mnaona?

144 Nina furaha sana usiku huu kumwona Ndugu Palmer, mmoja wa wachungaji wetu tunaoshirikiana nao huku, kutoka Georgia. Ndugu Junior Jackson yuko jengoni mahali fulani,

kule nyuma pembeni, tuna furaha kuwa pamoja naye. Ndugu Don Ruddell anayeketi hapa. Loo, wengi sana! Sijui, kama nikimkosa mtu ye yote . . . Ndugu Ben Bryant hapa, na wengi wa hao wengine hapa, ndugu mzuri, Wilbur Collins. Tuna furaha sana kuwa nanyi nyote hapa.

Sijui kama tu tungeweza kusimama kwa miguu yetu, kwa muda kidogo sasa. Hebu na tuviinamishe vichwa vyetu sasa.

> Hata twonane huko juu!
> Hata twonane Kwake kwema; hata twonane huko juu!
> Mungu awe nanyi daima.

145 Mnauhisi huo ushirika wa kuwa karibu na Roho?

Na tuuvumishe. [Ndugu Branham na kusanyiko wanaanza kuuvumisha *Mungu Awe Nanyi*—Mh.]

Nilimwona Ndugu McKinney, kutoka Ohio, akiwa pamoja nasi. Ndugu John Martin na ndugu yake. Nina furaha sana kuwa nanyi nyote. Huenda hata nisiwaone, ndugu. Yeye anawajua.

Hata twonane! Naomba kwamba moyo wangu na yenu, pamoja na moyo wa Mungu, uwe mmoja hata twonane! [Ndugu Branham na kusanyiko wanaendelea kuuvumisha *Mungu Awe Nanyi*—Mh.]

Tunapoviinamisha vichwa vyetu sasa katika maombi.

146 Jaribuni kumfanya kila mhudumu ajue ya kwamba tunafurahi kwa ajili yao kuwa hapa, washiriki wote, ninyi watu kutoka Tennessee, Ohio, na kila mahali nchini. Baadhi ya wanawake niliokutana nao kule leo, wametoka huko Boston. Ndugu zetu weusi walikuwa hapa, asubuhi ya leo, kutoka kule ndani pia. Wengi sana kutoka sehemu mbalimbali nchini; nawashukuru, marafiki zangu wapendwa na waaminfu. Mungu awe nanyi. Ninawaita ninyi rafiki zangu. Mnakumbuka vile Yesu alisema juu ya jambo hilo? "Wa karibu kuliko ndugu," naam, rafiki. Wakati tunapoviinamisha vichwa vyetu sasa . . . Hata tutakapokutana tena katika siku chache zijazo, Mungu awe nanyi.

147 Nitamwomba ndugu yetu mpendwa na mwaminifu, Ndugu Richard Blair, kama hataturuhusu tufumukane kwa maombi madogo. Ndugu Blair.

Wa Kipekee SWA64-0614E
(The Oddball)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili, tarehe 14 Juni, 1964, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1992 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org